# 13. Kununua na kuuza pembejeo za kilimo

## Mada ya 13b

# Udhibiti wa uwekaji wa pembejeo za kilimo

# JARIDA LA UHAKIKA

## 13. Kununua na kuuza pembejeo za kilimo

## Mada ya 13b: Udhibiti wa uwekaji wa pembejeo za kilimo

Kila biashara inayouza bidhaa lazima iweke bidhaa hizo. Wauza pembejeo za kilimo wanahitaji kuweka mbegu, mbolea, viuawadudu, na vifaa vya kilimo katika maduka yao. Kama **hakuna bidhaa**, hakuna kitakachouzwa na biashara itapoteza pesa. Kama **bidhaa nyingi zimewekwa**, bidhaa zinaweza kupitisha muda wa mwisho wa matumizi na zisiweze kuuzwa tena.

Ni muhimu kupata **kiasi sahihi cha bidhaa** cha kuweka cha kila bidhaa. Vipengele vifuatavyo huathiri kiasi sahihi cha bidhaa za kuweka:

1. Wakati wa msimu
2. Muda wa kungoja
3. Matakwa/haja ya wateja
4. Aina ya bidhaa
5. Kiasi cha bidhaa zinazouzwa kwa muda

**1. Wakati wa msimu**

Pembejeo za kilimo huuzwa tu wakati fulani katika msimu. Ni muhimu kujua mimea wanayoipanda wakulima na pembejeo zinazohitajika na mimea hiyo katika msimu.

**2. Muda wa kungoja**

Huu ni muda kati ya kuagiza bidhaa na kuvipata kutoka kwa mgawaji. Hutegemea uwezo wa mgawaji katika kugawa bidhaa/pembejeo.

- Kama muda wa kungoja ni **mrefu sana**, mwuzaji anafaa aweke bidhaa za kutosha ili bidhaa ziziishe kabla ya zingine kuwasili.
- Kama muda wa kungoja ni **mfupi sana**, mwuzaji anafaa aweke bidhaa za kutosha tu kwa muda mfupi kwa sababu anaweza kuagiza bidhaa zaidi kama anazihitaji na bidhaa zitawasili baada ya muda mfupi.

**3. Matakwa/haja ya wateja**

Mahitaji ya wakulima ya pembejeo za kilimo yatabadilika kulingana na yanayofanyika shambani. Wakulima hununua tu wanachohitaji, na wana pesa ya kukinunua. Kwa jumla, wakulima hushughulika tu kukiwa na shida badala ya kupanga mbele ili kuzuia shida. Kwa hivyo ni muhimu kuwafahamu wateja wako na kuwatafuta ili kujua ni nini watahitaji katika msimu ujao. Ni muhimu pia kujua kama aina fulani ya wadudu

waharibifu inatarajiwa. Maafisa wa nyanjani, vyama vya wauza pembejeo, au vyama vya wakulima vinaweza kusaidia.

**4. Aina ya bidhaa**

Aina fulani za pembejeo za kilimo zinaweza kukaa rafuni kwa muda mrefu. Bidhaa zingine hupitisha muda wa mwisho wa matumizi kwa haraka sana. Kumbuka yafuatayo unaponunua pembejeo za kilimo:

| Aina | Onyo | Mapendekezo |
|---|---|---|
| **Mbolea** | Ikiwekwa sana, mifuko ya plastiki inaweza kupasuka. Mbolea zingine huzeeka na kukosa nguvu sizipotumia kwa muda uliopendekezwa | Nunua tu pembejeo za kutosha msimu huo na uepuke kuweka bidhaa kwa mwaka mzima. |
| **Mbegu** | Mbegu zingine zina muda wa mwisho wa matumizi. Mbegu ambazo hazijatibiwa zinaweza kuvamiwa na wadudu waharibifu. | Nunua tu pembejeo za kutosha msimu huo na uepuke kuweka bidhaa kwa mwaka mzima. |
| **Viuawadudu** | Viuawadudu vina muda wa mwisho wa matumizi. Vyombo vya plastiki vya viuawadudu hubadili umbo vikiwekwa kwa muda mrefu. | Nunua tu pembejeo za kutosha msimu huo lakini weka bidhaa za dharura za wakulima. |

**5. Kiasi cha bidhaa kinachouzwa kwa muda fulali**

Ni kasi ambayo bidhaa zinabadilishwa katika pesa; yaani, ni muda kati ya kuweka bidhaa dukani na kuziuza. Katika uchuuzi rejareja, hili jambo ni muhimu sana.

- Kama kiasi hiki kinauzwa polepole, itachukua muda mrefu kabla ya pesa iliotumiwa kununua bidhaa kupatikana tena na hii pesa haiwezi kutumiwa kwa shughuli zingine hadi bidhaa zitakapouzwa.
- Kama kiasi hiki kinauzwa haraka, itachukua muda mfupi tu na pesa hiyo itumiwe tena kwa kununua bidhaa mpya au kuwekwa kama akiba.

Kama mwuzaji, inafaa uhakikishe kwamba bidhaa zinachukuwa muda mfupi sana kati ya kununuliwa na kuuzwa. Kufuata miongozo ilioko katika mada ya 2 ya dhamira IV kutakusidia kuhakikisha kwamba bidhaa ulizo nazo zinahitajika na wakulima.

**Muhimu:** Hali ya kila mwuzaji hutofautiana. Ni muhimu kwa mwuzaji kupanga ununuzi na uwekaji wa bidhaa kulingana na vipengele vilivyoko hapo juu.

# MWONGOZO

## 13. Kununua na kuuza pembejeo za kilimo

**Mada ya 13b:** Udhibiti wa uwekaji wa pembejeo za kilimo

**Vifaa vinavyohitajika:**

- ☑ Ubao ulio na makaratasi
- ☑ Markers (1 nyeusi, 1 bluu, 1 kijani, 1 nyekundu)
- ☑ Kadi za rangi
- ☑ Karatasi kubwa

**Muda unaohitajika:** Dakiki 30

**Maandalizi:**

- ☑ Makaratasi ya kufungua kurasa yalio na kichwa: *Udhibiti wa uwekaji wa pembejeo za kilimo*
- ☑ Karatasi lililo na kichwa: *Kiasi cha bidhaa* na *maandishi*:
  - *Wakati wa msimu*
  - *Muda kati ya kuagiza bidhaa na kuzipata*
  - *Matakwa/haja ya wateja*
  - *Aina ya bidhaa*
  - *Kiasi cha bidhaa kinachouzwa kwa muda fulani: muda kati ya kununua na kuuza.*

## Mwanzo

**U**sikivu: Uliza washiriki: Je, nyinyi huuza bidhaa zenu kwa siku moja? Jibu litakuwa: Hapana. Waambie kwamba, kwa hivyo itabidi waweke pembejeo za kilimo dukani. Lakini utajuaje kiasi sahihi cha kuweka?

**K**ichwa: Waambie kichwa ukiwaonyesha karatasi lililo na kichwa: *Udhibiti wa uwekaji wa pembejeo za kilimo.*

**K**usadikika: Elezea uzoefu wako katika biashara ya pembejeo za kilimo.

| | |
|---|---|
| **M**alengo: | Kuelezea vipengele muhimu vya kudhibiti uwekaji wa pembejeo za kilimo. |
| **M**anufaa: | Kujua bidhaa za kuweka dukani kutasaidia mwuza pembejeo kununua bidhaa sahihi, kuokoa pesa, na kutosheleza wakulima. |
| **M**welekeo: | Katika kipindi hiki, tutaangazia vipengele vya udhibiti wa uwekaji wa pembejeo za kilimo. Hatutajadili jinsi ya kuweka pembejeo kwenye ghala au jinsi ya kutabiri mauzo. Tutaangazia miongozo ya jumla ya kuweka pembejeo za kilimo. |

# Wasilisho

## **U**fafanuzi, **M**aonyesho, **M**azoezi, na **M**wongozo:

1. Bandika karatasi lililo na mchoro wa mti kwenye ukuta ambapo linaonekana na kila mtu. Waambie washiriki kwamba kama binadamu, mmea pia ina **sehemu mbalimbali** zilizo na kazi tofauti. Mmea ina sehemu tatu kuu: ya juu ya ardhi, ya chini ya ardhi na ya ndani ya mmea.
2. Waambie washiriki kwamba bidhaa zilizowekwa ni muhimu sana. Kama **hakuna bidhaa**, hakuna kitakachouzwa na biashara itapoteza pesa. Kama **bidhaa nyingi zimewekwa**, bidhaa zinaweza kupitisha muda wa mwisho wa matumizi na zisiweze kuuzwa tena. Ni muhimu kuweka kiasi kilicho sahihi cha kila bidhaa.
3. Waonyeshe karatasi lililo na kichwa: *Kiasi cha bidhaa zilizowekwa*. Waambie kwamba kuna vitu vitano muhimu vya kukumbuka unapodhibiti uwekaji wa bidhaa:
   - Wakati wa msimu
   - Muda wa kungoja
   - Matakwa/haja ya wateja
   - Aina ya bidhaa
   - Kiasi cha bidhaa zinazouzwa kwa muda
4. Eleza maana ya **muda wa kungoja** ambao ni muda kati ya kuagiza na kupokea bidhaa. Eleza maana ya kiasi cha bidhaa zinazouzwa kwa muda yaani kasi ya kubadili bidhaa katika pesa.
5. Gawanya washiriki katika vikundi vitano na upatie kila kikundi mojawapo ya vipengele vitano ili wavijadili. Kila kikundi kijadili **kwa nini kipengele hicho ni muhimu**. Kubali muda fulani kwa mjadala.
6. Jadili **matokeo**. Usiulize vikundi kuwasilisha majibu yao. Uliza tu kwa nini kipengele chao ni muhimu. Rudia kile kikundi kitasema na uulize vikundi vingine kama vinakubaliana. Ongeza hoja zako. Hakikisha umejadili hoja zote zilizotajwa kwa makaratasi ya vitendo.

# Malizia

**M**uhtasari: Peana muhtasari kwa kueleza kwamba vipo vipengele vitano muhimu vya kudhibiti uwekaji wa bidhaa: wakati wa msimu, muda wa kungoja, matakwa/haja ya wateja, aina ya bidhaa zinazowekwa, na kiasi kinachouzwa kwa muda/kasi ya kuuza. Eleza maana ya muda wa kungoja na kasi ya kuuza. Eleza ni kwa nini kila kipengele ni muhimu.

**M**aswali: Uliza kama kuna yeyote aliye na swali au maoni.

**T**athmini: Uliza washiriki kutaja vipengele vitano vya kudhibiti uwekaji wa pembejeo za kilimo. Waulize kufafanua muda wa kungoja. Uliza ni kwa nini ni muhimu kwa wauza pembejeo kujua watakachohitaji wakulima katika msimu ujao?

**H**atua fuatilizi: Tayari tumetaja katika kipindi hiki kwa nini ni muhimu kwa wauza pembejeo kujua watakachohitaji wakulima katika msimu ujao. Katika kipindi kitakachofuata, tutajadili kwa kina jinsi ya kutabiri mauzo.

Sambaza **makaratasi ya taarifa ya maelezo** kwa washiriki wote.